# Mieleweko Ambayo Lazima Isahihishwe

KIMEANDALIWA NA

**Prof/ Dkt. Abdullah Mabrouk Al Nagaar**

Mjumbe Baraza la Tafiti za Kiislamu

**Prof/ Dkt. Muhammad Salim Abu Aasi Mkuu Kitivo cha**

Masomo ya Juu, Chuo Kikuu Cha Al Azhar

KIMEREJEWA NA KUTOLEWANA

**PROF / DKT, MUHAMMAD MUKHTAAR JUMA**

**WAZIRI WA MAMBO YA WAOFU**

MJUMBE BARAZA LA TAFITI ZA KIISLAMU

Kimepitiwa Tafasiri ya kiswahili na
Profesa/ Ayman Alasar

Cairo 1436 AH/2015 CE

Shirika Kuu la Vitabu la Misri

مفاهيم يجب ان تصحح سواحيلي

Shirika Kuu la Vitabu la Misri

Mkurugenzi Mkuu.

Dr. Haitham Al-Haj Ally

# Mieleweko Ambayo Lazima Isahihishwe

MAANDALIZI

**DR. MOHAMMAD MUKHTAR JUMA**

**WAZIRI WA WAQFU**

Chapa ya kwanza

Shirikika Kuu la Vitabu la Misri 2021.

S.L.P235 Ramsis

1194 Kornesh Nail – Ramlatu Bolaq

Cairo.

Namba ya Post: 11794.

Simu: 202257775109 ndani 149

Fax: 20225764276.

Uchapishaji na utekelezaji

Kituo cha uchapishaji Shirika kuu la Vitabu nchini Misri

Mitazamo iliyopo ndani ya kitabu si msimamo wa shirika bali ni msimamo wa mtunzi kwa hatua ya kwanza.

Haki ya uchapishaji inalindwa na Shirika Kuu la vitabu la Misri. Ni marufuku kuchapisha au kusambaza au kutoa kopi au kuiga kwa hali yeyote ile isipokuwa kwa ruhusa ya Shirika Kuu la Vitabu la Misri au kwa maelekezo ya pande husika.

*Kwa Jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema Mwenye Kurehemu*

﴿**Na anacho kupeni Mtume chukueni, na anachokukatazeni**﴾ jiepusheni nacho

*Kwa Jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema Mwenye Kurehemu*

# UTANGULIZI

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, sifa zote njema ni za Mwenyezi Mungu rehema na amani zimwendee bwana wetu Mtume wa Mwenyezi Mungu pamoja na jamaa zake masahaba wake na wanaomfuata.

**Baada ya utangulizi huo:**

Kwa kupitia vyasia za Mkutano wa Kimataifa wa ishirini wa nne wa Baraza Kuu la Mambo ya Kiislamu, chini ya Wizara ya Wagfa, ambao ulifanyika kwa anwani; "Utakufu wa Uislamu na Makosa ya Wanaojinasibisha nao, njia ya Kusahihisha", tuna furaba ya kumletea ndugu msomaji yale yaliyoandikwa na Prof/Dkt, Abdullah Mabrouk Al Nagaar. Mjumbe wa Baraza la Tafiti za Kiislamu. Na Prof

/Dkt. Muhammad Salim Abu Aasi, Mkurugenzi Mkuu wa Kitivo cha Masomo ya Juu, Chuo Kikuu Cha Al Azhar, katika maelezo na ufafanuzi wa nyasia hizo.

Ni matumaimi yetu kuwa tutasahihisha baadhi ya fikra potofu na zenye makosa na zilizopotoshwa, ambazo zinaweza zikapelekea baadhi ya matumizi ya nguvu, au kuelekea katika kukufurisha au misimamo mikali, tunatarajia kwamba kijitabu hichi kiwe ni mwanzo wa mfululizo wa machapisho mengine yahusiyo usahihishaji wa mieleweko mbalimbali, na kueneza usamehevu wa Uislamu, na kudhihirisha pande mbalimbali za ustaarabu wake uliopevuka ambao unaweka misingi imara ya majadiliano ya kistaarabu na kuishi pamoja kwa amani kati ya wanadamu wote, pamoja na kueneza maadili bora na ya kibinadamu kwa njia ambayo inaleta furaha kwa watu wote ulimwenguni,

*Waziri wa Mambo ya Wagfu*

***Profesa Dkt. Muhammad Mukhtaar Juma***

***

## Nyasia za Mkutano wa Kimataifa wa Ishirini na nne wa Baraza Kuu la Mambo ya Kiislamu. Ubainishaji na Uchambuzi

Chini ya ulezi wa Rais Abdulfatah Al Sisi, Rais wa Jamhuri ya Kiarabu ya Misri, na chini ya uwenyekiti wa Prof Dkt. Muhammad Mukhtar Juma, Waziri wa Mambo ya Wakfu na Mwenyekiti wa Baraza Kuu la Mambo ya Kiislamu, wanachuoni vigogo wa Umma wa Kiislamu na wanafikra, wa madhehebu mbalimbali ya kifikra na ya kidini, walikutana kwenye Mkutano Mkuu wa Kimataifa wa Ishirini na nne wa Baraza Kuu la Mambo ya Kiislamu na kudurusu wakati wa vikao vyao yale yanayotokea katika ulimwengu wa Kiislamu kwa wakati huu wa hivi mwishoni miongoni mwa mizozo ya kisiasa ya kiusalama na ya kifikra ambayo ilisababisha utekelezaji wa kimakosa, na matukio ya kuhuzunisha kama vile ukafirishaji, ugaidi na matumizi ya nguvu... na mengine men-

gi, jambo ambalo linatishia amani ya kimataifa, na kushambulia utulivu wa jamii nyingi za kibinadamu kwa kuziingiza katika machafuko ya kudumu yenye kuangamiza na matumizi ya nguvu ambayo hayabakishi kitu wala hayasanzi.

Na wote waliokutana walisisitiza kuwa miongoni mwa mambo yaliyoongeza hali kuwa mbaya zaidi katikati ya uhalisia huu wenye kutia uchungu na ambayo umma wa Kiislamu unaoishi hii leo kama vile kuvurugwa mieleweko sahihi na kugeuzwa ukweli wa mambo yaliyo thabiti, ni vita vya baadhi ya makundi yaliyodanganyika na ambayo yanajinasibisha na Uislamu kwa dhuluma, na kwa kila njia ili kuzidisha farakano na kuongeza pengo lililopo, na kuanzisha mgawanyiko, na kupanua zaidi ukiukaji, na kujaribu kubadilisha matini za kisheria kwa namna ambayo inakubaliana na fikra zao wanazozidai, na rai zilizopotoshwa, na kujenga sura kwa watu kuwa hiyo ndiyo sahihi na ukweli uliowazi.

Kutokana na jukumu la kisheria la kitaifa na la kibinadamu ambalo wanachuoni pamoja na wanafikra wamebebeshwa, na kutokana na wao kuamini udharura wa kupambana kielimu na fikra potofu, na mieleweko ya kimakosa kuhusu masuala mbali mbali kama vile Jihadi, Ukafirishaji, mfamo wa kutoa maamuzi, uraia na mengi mengineyo…, na kufanya kazi ya kuwafichua baadhi ya wanaojinasibisha kidini na Uislamu kwa malengo ya kujinufaisha au madaraka ili wayafikie malengo yao machafu, Mkutano ulitangaza Jumla ya nyasia kama ifuatavyo:-

1- Mkutano unatangaza kuwa Uislamu ni dini inayoulea Uhuru wa Imani/Itikadi kwa tamko lake Mwenyezi Mungu {Hakuna kulazimishana katika Dini} na kwamba Uislamu unawasawisha watu wote kafika Utaifa, Haki zote na wajibu bila kujali tofauti zao za kiitikadi na bila ubaguzi wowote, na kwamba nguzo yake ni Uadilifu, Huruma na ni Utunzaji wa maadili mema na kuyalinda kwake, na unak-

ubali tofauti za watu kwa kuzingatia kuwa ni siri ya Ulimwengu. Uislamu pia unaharamisha kuwashambulia watu, heshima na mali zao, isipokuwa kwa kujibu mashambulizi ya wazi dhidi ya nchi yao , na kwa mujibu wa maamuzi ya rais wa nchi hiyo na taasisi zinazohusika na jambo hilo ndani ya nchi, kwani kutangaza vita kwa ajili ya ulinzi wa Mataifa ni haki ya kila nchi kwa mujibu wa maamuzi ya katiba ya nchi hiyo na rais wake, na wala si haki ya kila mtu, na kwamba Uislamu unaheshimu akili kama ni chombo cha kutia fikra sahii na kutosheleza undani wa mtu na hukuza hisia pia hukutanisha kati ya Dunia na Akhera, na kila kitendo kinachofanyika bila yake ni kinyume na Uislamu ulio sahihi.

2- Uislamu hauna hatia yeyote kwa yale wayatendayo baadhi ya wanaojinasibisha nao, kwa kukufurisha au kuandaa baadhi ya vitendo vya kihalifu juu ya Uislamu, kama vile kuchinja watu, kuwachoma moto au kuwafanyia un-

yama, kuangamiza au kufanya uharibifu wowote, kwani yote hayo ni kuzusha dhidi ya haki ya Mwenyezi Mungu, na aliye mjuzi pekee wa yaliyomo ndani ya nyoyo za waja wake, na pia ni uzushi dhidi ya haki ya Kiongozi muhusika.

3- Haifaihi kuuingiza Uislamu kutokana na makosa ya baadhi ya wanaojinasibisha nao, na wala haifai kutokana na kuelewa kwao kimakosa au kwenda kinyume na mfumo wake.

4- Wafuasi wote wa dini nyengine wanapaswa kuziangalia dini nyingine kwa kigezo kimoja kilicho adilifu bila ya kuzibebesha jukumu la makosa ya baadhi ya wafuasi wake.

5- Kuitumia Dini kunakofanywa na Baadhi ya wanaojinasibisha nayo kwa malengo ya kujinufaisha au kutaka cheo ni kuitendea vibaya na ni kufanya makosa dhidi ya haki ya Dini hiyo.

6- Wanachuoni wote pamoja na wanafikra, watafiti na waandishi wa vitabu wamekubaliana

kupinga watu kufukuzwa na kutolewa katika nchi zao, au kuwabomolea majumba yao ya ibada, kuwateka wanawake wao na kuhalalisha mali zao kwa sababu tu ya tofauti ya dini yao chini ya kile kinachoitwa Dola la Kiislamu au kwa jina lolote lengine liwalo, na Uislamu hauhusiki na hayo yote.

7- Wote waliokutana walikubaliana kuharamisha chuki za kidini ukiwemo ushambuliaji wa hisia za wafuasi wake, pia kutokana na yale yanayojitokeza kwa hali hiyo kama vile kuvuruga mfumo wa kijamii na wa kibinadamu kwa ujumla, vile vile kutokana na kueneza uchochezi, vurugu na ukinzani wa staarabu.

8- Wote waliohudhuria mkutano walikubaliana kusahihisha mieleweko ifuatayo:-

**A.** Ugaidi: Nao ni uhalifu wa kupangwa ambao hulihusisha kundi la watu waliojiengua katika mfumo wa nchi na jamii, na hufanikiwa

kutokana na uhalifu huo, kumwaga damu ya wasio na hatia au kuharibu taasisi au kushambulia mali za umma au watu binafsi.

**B.** Ukhalifa: Ni sifa ya hali ya utawala wa kisiasa unaobadilika na ambao nafasi yake inaweza kuendeshwa kwa mfumo wowote wa kisiasa utakaofanikisha masilahi ya nchi na wananchi kwa mujibu wa wigo wa sheria na mikataba ya kimataifa, na Aya zilizopokelewa juu yake zinaonesha kuwepo unyeti wa kupatikana kwa mfumo ambao una kiongozi na taasisi mbalimbali ili watu wasiishi katika hali ya vurugu, kwa hivyo basi kila aina ya utawala unaotumikia masilahi ya nchi na wananchi na kuweka uadilifu basi ndio utawala bora na kwa mujibu wa hivyo, basi si haki ya mtu yeyote au kikundi chochote kumsindika Khalifa madarakani au kudai nchi ya kikhalifa nje ya mfumo wa demokrasia za kisasa.

**C.** Kodi: Ni jina la uwajibikaji wa kifedha ambalo katika zama zetu uwajibikaji nalo haupo tena, na sababu zake zimetoweka kwa kutoweka kile kilichopelekea kisheria kuwepo kwake katika wakati wake, kwa kuwa wananchi wote wamekuwa sawa sawa kwa haki na kwa uwajibikaji, na sehema yake ikachukuliwa na vidhibiti vya mifumo mengine ya kifedha, na kupelekea kutoweka kwa sababu ya kuwepo kwake, na maelezo yaliyopokelewa ndani ya Quran kuhusu jambo hili yanawaelekea maadui wapiga vita Uislamu na washambuliaji, tena wanaoukataa utaifa wao, na sio kwa wananchi walio na amani wasioupiga vita Uislamu na wanaoshiriki katika ujenzi wa nchi pamoja na kulinda nchi hiyo.

**D.** Nchi ya adui: Huwa ni msamiati wa kigeni unaobadilika, na kwa wakati wetu wa sasa, haupo tena kwa maana ya kiistilahi ya

kale kwa kuwepo mikataba mbalimbali ya Kimataifa ya nyaraka za umoja wa mataifa, na kuubadilisha kwake kwa hakika wala hakuendi kombo dhidi ya nchi mbalimbali katika kuzirejesha ardhi zake zilizonyakuliwa, na hasa hasa haki za wananchi wa Palestina, na Sharia ya Kiislamu inayowajibisha utekelezaji wa mikataba, na kutokana na hivyo, hakuna uhamiaji kutoka nchi fulani kwa madai kuwa eti kuvamia kwenye nchi ya Kiislamu.

**E.** Utaifa: Neno hili lina maana kuwa wananchi wote ni sawa kwenye haki na wajibu ndani ya mipaka ya nchi yao wote.

**F.** Jihadi: Vita: Kwa kujibu mashambulizi dhidi ya nchi kwa kiwango kinachofanana bila ya kupindukia au kupunguza, na hakuna nafasi ya kushambulia nchi yeyote wala si haki ya mtu yeyote kutangaza vita, kwani hii ni haki ya rais wa nchi pamoja na pande husika na kwa mujibu wa kanuni na katiba ya nchi.

**G.** Ni juu ya taasisi za Kielimu na Kidini kuweka vigezo vya ukafirishaji ili mahakimu wawe navyo, na kwa namna ambayo inajenga mzinduko wa kiutamaduni na kijamii unaotenganisha kati ya yale yanayowezekana kumfikisha mtu kwenye ukafiri na yale ambayo hayamfikishi huko. Ama kwa upande wa hukumu ya watu au mashirika au makundi mbalimbali haiwi haki ya watu, mashirika au makundi mbali mbali, bali hawa kwa mujibu wa hukumu ya kimahakama yenye kuzingatia vigezo vya dalili zake za kisheria na vigezo ambavyo huwekwa na taasisi za kidini zinazokubalika, ili zisitokee vurugu za kukafirishana, pamoja na kuwepo sisitizo kuwa uhalalishaji wa mauaji ya binadamu, kuwachinja, kuwachoma moto, au kuwaadhibu ambako kunafanywa na baadhi ya watu, makundi au mashirika, kunazingatiwa kuwa ni kutoka nje ya Uislam.

**H.** Hakimiya: Ni neno lenye maana ya uwajibikaji wa Sharia aliyoiteremsha Mwenyezi

Mungu Mtukafu, na jambo hili halizuii maamuzi ya wanadamu kwa kutenda sheria walizozitunga wenyewe ndani ya msitari wa msingi wa sheria mama na nguzo zake kuu kwa mujibu wa mabadiliko ya zama na sehemu pia za utumiaji wa sheria hizo za kutungwa huenda kinyume na sheria ya Mwenyezi Mengu kwa kuwa tu unayatumikia maslahi makuu ya nchi, mataifa, watu na jamii mbali mbali kwa mujibu wa makusudio makuu ya Mfumo wa Sharia ya Kiislamu.

9- Kuna umubimu wa kuboresha mfumo wa ulinganiaji wa Kiislamu kwa namna ambayo ulinganiaji huo unakuwa na uwiano unaokusanya akili na unukulu na maslahi ya mtu, jamii na nchi, na unaleta usawa wa haki na wajibu kwa mwanamke na mwanaume, na mnakuwa na uwezo wa kupambana na kila aina ya mlengo mkali, kujikweza, ulegevu na ukafiri.

10- Wote waliokutana wanausia kuundwa kwa kituo cha ufuatiliaji cha kudumu kwa lugha

zote za Kimataifa, ambapo kazi yake itakuwa ni kufuatilia makosa ya baadhi ya wanaojinasibisha na Uislamu na kuwajibu kwa hoja na dalili, kwa namna ambayo kitengo hicho kitaunganisha kati ya mamlaka na taasisi zote za Kiislamu ulimwengu.

11- Ni lazima kuangalia upya mitaala ya masomo ya kidini na ya kitamaduni katika taasisi zote za elimu katika ulimwengu wa Kiarabu na wa Kiislamu, na kuisafisha kutokana na mambo yote yanayohusiana na hali za kihistoria, zama na sehemu maalumu, jambo ambalo linahitaji kutazamwa upya ndani yake kwa mujibu wa hali zetu, zama zetu na sehemu tulipo kwa namna ambayo itapelekea kaeneza utamaduni wa usamehevu, na kuiunda akili kwa mamna ambayo itaifanya kuwa na uwezo wa kufikiri na kutoa maamuzi ya kisheria juu ya mapya na yajitokezayo bila kudharau uhalisia wake au kwenda kinyume nao.

12- Wote wanataka kuchangamsha wito wa Mheshimiwa rais wa Jamhuri ya Kiarabu ya Misri, akiwa kama mlezi wa mkutano, rais Abdulfatah Sisi, wa kutaka mataifa ya kiarabu yaunde jeshi la pamoja la kujihami kwa ajili ya kupambana na ugaidi.

13- Wote wanataka zichukuliwe hatuwa na nchi za Kiarabu na za Kiislamu kuelekea katika uundaji wa jumuiya za kisiasa, kiuchumi, kifikra na kiutamaduni chini ya kivuli cha Jumuiya ya Nchi za Kiarabu na Jumuiya ya Nchi za Kiislamu, (OIC)

kwa mamba ambayo itaunda jamii kubwa na yenye nguvu ambayo ni vigumu kupenya na kuigawa ndani ya majukwaa ya kimataifa au Jumuiya za Kiuchumi za Kimataifa, au vita vya kifikra na vya kitamaduni kwa wananchi wa Kiarabu na Kiislamu.

14- Kuratibu kati ya Wizara zinazohusika na utamaduni na elimu, elimu ya juu, utamaduni

na vijana, kama kikosi kazi, na vyombo vya habari vitoe mchango wake wa kuweka misingi imara na maadili bora.

15- Kuusia shime ya hali ya juu ya kutoa mafunzo na kutamadunisha, kwa kutumia njia za kisasa za mawasilano na hata katika taasisi za kidini, kifikra na kitamaduni.

16- Wote walikubaliana uundwaji wa kamati ya kufuatilia utekelezaji wa nyasia na ambayo itakuwa ikikutana kila baada ya miezi mitano na akutoa taarifa ambayo itakuwa ikitumwa kwa washiriki wote na kwa vyombo mbalimbali vya habari, ili kuzungumzia yaliyokwishatekelezwa.

***

## Dibaji.

Kabla ya hatujaanza kufafanua na kuchambua wasia wa nane ambao ndani yake ulizungumzia sisitizo juu ya kusahihisha baadhi ya mieleweko yenye makosa, tuanze na wasia wa kwanza, kwa ajili ya umuhimu wake katika kusahihisha sura ya Uislamu iliyochafuliwa, ambapo huu mkutano ulitangaza katika wasia wake wa kwanza kwamba Dini ya Kiislamu inadhamini uhuru wa Itikadi, na unasawisha watu wote katika haki na wajibu, pamoja na kuwepo tofauti ya imani zao, bila ya ubaguzi, na kwamba msingi wa Uisamu ni uadilifu na huruma na kuhifadhi thamani ya maadili na kulinda, kukubali uwepo wa tofauti na kuuzingatia kuwa ni siri ya Ulimwengu, pia Uislamu unatahadharisha kuua, kuvunja heshima na kushabulia mali za wengine isipokuwa kwa ajili ya kuurudisha uadui wa wazi juu ya nchi ya Kiislamu, na kwa mujibu wa maamuzi ya rais wa nchi hiyo

pamoja na pande zote zinazohusika na jambo hilo, Kwa hivyo basi, kutangaza vita kwa ajili ya kujilinda ni haki ya nchi na kwa mujibu wa katibu yake na rais, na wala si haki ya kila mtu.

**Na ufafanuzi wake katika yafuatazo:**

Uislamu umekuja ni uwe rehema kwa watu wote ulimwenguni, na ili kuondosha minyororo na shida mbalimbali za wanadamu wote, Na katika sheria zake zenye hekima na mafunzo yake matukufu yenye muonekano mzuri na huruma pamoja na usamehevu kwa wasio Waislamu.

Kwani Aya za Quran Tukufu zimethibitisha hayo na kwamba miongoni mwa Sunna za Mwenyezi Mungu Mtukufu katika viumbe wake ni tofauti za maumbile yao na lugha zao kama vile zilivyo tofauti za dini zao, na kwamba tofauti hii itaendaelea kuwepo kwa kuwepo mwanadamu juu ya ardhi hii, kama alivyosema Mwenyezi Mungu Mtukufu: ﴿**Na Mola wako Mlezi angelipenda angewafanya watu wete wakawa umma mmo-**

**ja. Lakini hawaachi kukhitalifiana. Isipokuwa wale ambao Mola wako Mlezi amewarehemu, na kwa hiyo ndio Mwenyezi Mungu amewaumba. Na litatimia neno la Mola wako Mlezi, Kweli kweli nitaijaza Jahannam kwa majini na watu pamoja**﴾ HUD: 1118, 1151.

Na haikubaliki pamoja na tofauti hii ya watu kwamba jamii ya Kiislamu ijitenge na jamii zote nyengine, kwa hiyo Uislamu umekuja ili kupanga uhusiano wa Muislamu pamoja na wanadamu wengine miongoni mwa Waislamu na wasio Waislamu, na hukumu za Kiislamu katika matendeano pamoja na wasio Waislamu na dini na aina zao tofauti miongoni mwa watu wa Kitabu (Wakristo na Wayahudi) zilikuwa dalili tosha na alama ng'avu za kwamba Uislamu unamheshimu mwengine na aliyetofauti.

**Miongoni mwa hukumu hizo:**

Kwamba Uislamu unadhamini uhuru wa kuabudu wa kila mtu, na kwa hivyo basi, hakuna kulazimishwa mtu kuingia katika Uislamu isi-

pokuwa ni kwa kukinaika kikamilifu na muongozo wa Uislamu, kwa hivyo basi kila mtuo ana dini yake na halazimishwi kuiacha ili aingie kwenye dini nyengine. Qurani Tukufu inaelezea katika Aya zake maana hiyo, katika kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukafu: ﴿**Hapana kulazimisha katika Dini, Kwani Uoongofu umekwisha pambanuka na upotofu**﴾ Al-Baqarah: 256.

Na Mtume S.A.W amekataza kuwalazimisha watu kuingia katika dini hii kwa kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu katika Surat Yunus iliyoteremshwa Makkah: ﴿**Angelitaka Mola wako Mlezi wangeamini wote waliomo katika ardhi. Je, wewe unawalazimisha watu kwa nguvu mpaka wawe Waummi**﴾ Yunus: 59.

Na Sharia za Uislamu zinawajibisha Waishimu wote kuwa na mwenendo wa uadilifu katika kutendeana na wengine, na wala hazijafanya tofauti katika dini kuwa ni sababu ya kudhulumu au kuwashambulia wengine, bali zimefanya uadilifu kwa wengine kuwa ni dalili ya Ucha-Mungu ambao umepangiwa juu yake thawabu za juu mno,

kama alivyosema Mwenyezi Mungu Mtukufu: ﴿**Enyi mlio amini! Kuweni wasimamizi madhubuti kwa ajili ya Mwenyezi Mungu mkitoa ushahidi kwa haki, wala kuchukiana na watu kusikupelekeeni kutofanya uadilifu, fanyeni uadilifu, hivyo ndio kuwa karibu mno na Ucha-Mungu**﴾ Al-Maidah: 08.

Kwa hivyo basi, amri ya kuwafanyia uadilifu watu wote ni ya kutekelezwa bila kujali nafsi zao aina zao dini zao au nasaba zao.

**Na dalili juu ya hayo ni:**

Kwamba Mwenyezi Mangu Mtukufu alimuamuru Mtume wake S.A.W kuhukumu kwa uadilifu pale walipomjia watu wa Kitabu wakamuomba awahukumu kati yao, na Mwenyezi Mangu Mtukufu Anasema: ﴿**Na ukiwahukumu, hasi hukumu kati yao kwa uadilifu. Hakika Mwenyezi Mungu anawapenda waadilifu**﴾ Al-Maidah: 42.

Bali Mtume S.A.W alitilia mkazo juu ya onyo kali kwa atakayemdhulumu mtu mwenye ahadi, na akasema Mtume kuwa Yeye atakuwa mgomvi

wake siku ya Kiyama. Na hakuna shaka kuwa mtu yeyote ambaye ni mgomvi wa Mtume S.A.W. basi atatoka patupu na atapata hasara kubwa, Mtume S.A.W amesema: "Isipokuwa aliyemdhulumu mtu mwenye ahadi au kumpunguzia haki yake, au kumkalifisha nje ya uwezo wake, au kuchukua kitu chake chochote bila ya ridhaa yake, basi mimi nitakuwa mgomvi wake na nitahojiana naye siku ya Kiyama«. Hadithi imepokelewa na Abu Dawud.

Na katika Quran kuna Aya nyingi zinazoamrisha kutenda mazuri, uhusiano bora wema uadilifu na kutekeleza ahadi, na kuna Aya nyingi zinazomgusa kila mtu, kwani Mwenyezi Mungu Mtukufu Anasema: {Na fanyeni wema, Hakika Mwenyezi Mungu huwapenda wafanyao wema} AI-Baqarah. Na Akasema: ﴿**Na semeni na watu kwa wema**﴾ Al-Baqarah: 83.

Na kwenye dhana jumla ya wema huu; Uislamu unaamrisha kuwatendea wema wasio Waislamu ambao hawakuwafanyia maudhi Waislamu pamoja na kuwapiga vita kwani Mwenyezi Mungu Mtu-

kufu Anasema: ﴾**Hakika Mwenyezi Mungu hakukatazeni kuwafanyia wema na uadilifu wale ambao hawakukupigeni vita, wala hawakukutoeni makwenu. Hakika Mwenyezi Mungu huwapenda wafanyao uadilifu**﴿ Al- Mumtahina: 08.

Kama vile, Uislamu unahalalisha kushirikiana pamoja na wasio Waislamu katika kuuza na kununua kuchukuwa na katoa, na ukahalalisha chakula cha watu wa Kitabu, na umeamrisha kuwatendea wema, pia Uislamu ulibeba jukumu la kudhamini usalama wa wasio Waislamu katika jamii ya Kiislamu, usalama wao, mali zao na heshima zao, kwa hivyo Uislamu haukubali mtu yeyote asiye Muislamu kuudhiwa iwe na Muislamu au mtu mwingine yeyote.

Na Uislamu umetoa onyo kali na kuweka adhabu nzito kwa mtu atakayehalalisha mauaji ya wasio Waislamu au kuudhiwa. Mtume S.A.W Anasema: "Aliyemuua mwenye ahadi hatanusa harufu ya peponi na kwamba harufu yake hiyo inapatikana kwa umbali wa mwendo wa miaka arubaini". Imepokelewa na Imamu Bukhariy.

Na kwa hivyo, historla haijapata kuujua umma wowote miongoni mwa umma mbali mbali, ambao uliwafanyia hivyo wakinzani wao katika dini yake, pia vile vile uliwatendea wananchi wake na wale wote wanaojinasibisha nao katika suala la Sharia za kiadilifu na mazuri katika maisha yao kwa msingi ujulikanao: "Lao ni letu wajibu wao ni wajibu wetu" pamoja na kuendelea kubakia katika dini, mila na desturi zao kama vile ulivyokuwa umma wa Kiislamu, na kama haya yana maana basi maana yake ni utukufu wa Uislamu ambao unaonekana wazi kwa usamehevu wake kwa namna ambayo inaondosha madai yote yaliyo batili ambayo kwayo maadui wanajaribu kuyaunganisha na Uislamu wakizingatia kuwa Uislamu ni dini ya ugaidi ubabe na uvivu uliopindukia, kinyume na sifa za usamebevu na huruma ambazo Uislamu unasifika kwazo.

***

# Kuainisha Mieleweko na Vigezo vyake vya Kisharia

## Kwanza: Ukafirishaji.

Mkutano wa Kiislamu uliusia kuwa: Taasisi zitoazo elimu ya dini zinapaswa kuweka vidhibiti vya ukafirishaji ili uwe mikononi mwa makadhi (Mahakimu wa Kiislama) na kwa namna ambayo inaunda mwamko wa kiutamaduni na kijamii, unaotofutisha kati ya kile kinachoweza kumfikisha mtu kwenye ukafiri, na kila ambacho kakimfikishi huko.

Kwa upande wa kuwahukumu watu, mashirika au makundi, haikuwa ni haki ya watu, mashirika au makundi, bali kunakuwa kwa mujibu wa maamuzi ya kimahakama kwa vigezo vya kidini vinavyokubalika ili tusije kuangukia kwenye zogo la kukafirishana.

Pamoja va kusisitiza kuwa uhalalishaji wa mauaji ya watu, kuwachinja, kuwachoma moto au hata kuwaadhibu, kunakofanywa na watu, makundi au mashirika, kunazingatiwa kuwa ni kujitoa katika Uislamu.

**Na katika nfafanuzi wa hayo tunasema:**

Ukafirishaji ni kumuhukumu Muislamu kuwa yeye ni kafiri, na kumuhukumu Muislamu kuwa ni kafiri ni jambo la hatari mno linasababisha athari duniani na akhera.

Na miongoni mwa athari za kidunia: Ni kuwatenganisha mume na mkewe, na watoto kutokuwa chini ya uongozi (ulezi) wa baba yao, na kukosa haki ya uongozi na nusra kwa jamii ya Kiislamu, na kumuhukumu mbele ya makadhi (Mahakimu wa Kiislamu) na katotunia hukumu za

Waislamu juu ya mtuhumiwa, kwa hivyo anapofariki haogeshwi na Waislamu wala kuswaliwa, na wala hazikwi katika makaburi yao, pia harithi wala harithiwi.

Na miongoni mwa athari za akhera: Iwapo mtu atakufa na ukafiri wake basi anastahiki laana ya Mwenyezi Mangu na kufukuzwa katika rehema zake, na kuishi maisha ya motoni milele.

Anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu: ﴿**Hakika walio kufuru na wakala wakiwa makafiri, hao iko juu yao laana ya Mwenyezi Mungu na ya Malaika na ya watu wote, watadumu humo motoni. hawatapunguziwa adhabu wala hawatapewa muda wa kupumzika**﴾ Al-Baqarah: 1561-162

Na anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu: ﴿**Hakika Mwenyezi Mungu hasamehe kushirikishwa, na husamebe yaliyo chini ya hilo kwa amtakaye. Na anayemshirikisha Mwenyezi Mungu basi hakika amezua dhambi kubwa**﴾ An Nisaa: 48.

Na kwa ajili hii, mtu anayeingia katika utoaji wa kukamu ya ukafirishaji anapaswa awe muangalifu mno katika maamuzi yake kwa kuangalia mara kadhaa kabla ya kupitisha maamuzi hayo.

Na kutokana na hatari ya ukafirishaji juu ya jamii, Uislamu unapinga kuharakisha maamuzi yake, au kuukubali isipokuwa baada ya kuuthibitisha kwa sababu zake za wazi na zisizo na shaka yeyote, kwani mwanadamu akikosea katika usamehevu ni bora zaidi kuliko kukosea katika adhabu, na rejeo lake katika jambo hilo kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu,

Quran Tukufu imelalamika kuhusu Usama Ibn Zaid Swababa wa Mtume S.A.W. kumuua mtu aliyemsalimia naye na ilimuamuru na kutuamuru sisi sote kuhakikisha katika kauli ya Mwenyezi Munzu Mtukufu ﴿**Enyi mlio amini! Mnapo safari katika Njia ya Mwenyezi Mungu basi hakikisheni, wala msimwambie anayekutoleeni salamu: Wewe si Muumini kwa kutaka manufaa ya maisha ya dunia hii, bali ya kuwa kwa Mwenyezi Mungu zipo ghanima nyingi. Hivyo ndivyo mlivyo kuwa nyinyi zamani, na Mwenyezi Mungu akakuneemesheni, Basi chunguzeni sawa sawa. Hakika Mwenyezi Munga anazo habari za mnayo yatenda**﴾ An Nisaa: 94.

Na Miume S.A.W alionya kwa nguvu ukafirishaji na akasema: "Mtu yeyote atakayemkafirisha mwenziwe basi atakuwa amerejea katika ukafiri wa mmoja wao". Imekubalika na Maimamu wa Hadithi.

Na Wanachuoni walielewa hatari ya kutoa hukumu ya kukafirisha, na wakaogopa kuharakisha kutamka hukumu hiyo isipokuwa kwa dalili ya wazi, na ufafanuzi wa wazi, kwani ushahidi wa kukufuru kwa Muislamu ni uzushi, udhalimu na urongo wa hali ya juu.

Na Maswahaba Watukufu R.A walikuwa wakijizuia kutoa tamko la ukafiri au ufuska kwa Muislamu yeyote, na kutoka kwa Abu Sufian alisema: "Nilimwambia Jaber: Je, mlikuwa mkimwambia Muislamu yeyote kuwa kafiri? Akasema: Hapana. Nikasema: Na mshirikina je? Akasema: Audhubiliahi! Najikinga na Mwenyezi Mungu na akafadhaika". Imepokelewa na Ibn Abduibar katika kitabu cha Al Tamheed 17/21.

Na Ali Ibn Abi Twalib R.A alipoulizwa kuhusu khawariji Je, wao ni washirikina? Akasema: "Hapana, wao wamekimbia ushirikina. Na pakaulizwa: Je wao wanafiki? Akasema: Hapana, kwani wanafiki hawamtaji Mwenyezi Mungu Mtukufu isipokuwa kidogo, pakaulizwa: Na je nini basi hali yao? Akasema wao ni ndegu zetu waliotudhulumu. Basi wao ni madhalimu wanapigana vita vya watu wa dhuluma ili kuwarudishia udhalimu wao". Al-Jaamiil ahkaami Al-Ouran 324/16.

Kwa hivyo, tunatakiwa kutoharakisha katika kumkafirisha mtu yeyote, na kama baadhi ya makundi yanawakafirisha wanaopingana nao, basi sisi hatuwakafirishi isipokuwa wakihalalisha damu za watu, mali na heshima zao bila ya haki.

Al-Shaukany Rehema ya Mwenyezi Mangu ziwe juu yake amesema! "Elewa kuwa hukumu juu ya Muislamu kuwa ameacha Uislamu na kuingia ukafiri. Muislamu anayemuamini Mwenyezi Mungu na siku ya akhera, haifai kusemwa ila kwa dalili

iliyo wazi zaidi ya jua la mchana, kwani imethibitika kwa Hadithi sahihi zilizopokelewa kwa njia ya kundi la Masahaba kuwa "Mtu yeyote atakaye mwambia Muislamu mwenzake: Ewe kafiri! Basi atakuwa mmoja wao", basi katika Hadithi hizo na nyenginezo nyingi kuna karipio kubwa mno na mawaidha ya kutosha kwa yule anayeharakisha kutoa hukumu ya ukafirishaji, As Saili Al-Jaraar 578/4.

Na imenukuliwa kutoka kwa Imamu Maliki Rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake "Kuwa mtu ambaye itaonekana kutoka kwake dalili tisini na tisa za uwezekano wa kuwa kafiri na pakawepe dalili moja tu ya kuwa kwake Muislamu basi atazingatiwa kuwa ni Muislamu".

Na Kigogo cha Uislamu, Al-Imamu Al-Ghazaliy Rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake alisema: "Na anachopaswa kukiegemea yule anayeliangalia kwa undani jambo hili ni kujiepusha na ukafirishaji pindipo atakapopata njia ya kufanya

hivyo, Kwani kuhalalisha damu na mali za wanaoswali wakielekea Qibla na wanaoshuhudia kwa kauli ya "Hakuna Mola isipokuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu na kuwa Muhammad ni Mtume wake" ni kosa kubwa, na kosa la kuwaacha makafiri elfu moja maishani ni jepesi kuliko kosa la kumwagika damu ya jeraha la Muislamu". AI-Iktiissadi Fiy Al Wikaadi Uk.135.

Na anasema Rehema ya Mwenyezi Mangu iwe juu yake "Wasia ni kuuzuia ulimi wako dhidi ya watu wa Qibla kwa namna uwezavyo kufanya hayo, iwapo tu watu hao wanaendelea kusema: Hakuna Mola isipokuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu na kuwa Muhammad ni Mtume wake, na wao hawapingi maneno haya". Faiysai Al-Tafrugah kati ya Uislamu na Uzindiki, Uk: 128.

Al-Imamu Al-Bajuriy amewazungumzia Khawarij kwa kusema: "Na wala hawakukufuru kwa kumkufurisha mwenye kufanya madhambi, pamoja na kwamba aliyemkufurisha Muislamu

naye pia amekufuru kwa sababu wao wamesema hivyo kwa kutafuta maana na kwa kujitahidi". Hashiat Al-Baijuriy Al-Sharh Al-Jawharal.

Na katika misingi ya asili iliyokubalika kwa Ahlu Sunna Wal Jamaa ni kwamba: Haifai kumuhukumu Muislamu kuwa ni kafiri hata kama kutakuwa na viashirio vingi vinavyounga mkono hukumu hiyo juu ya Muislamu huyo kwa kuwa kuna uwezekano mmoja tu wa kuendelea kubakia kwake katika Uislamu.

Lakini fikira ya ukafirishaji inaakisi hukumu hiyo, basi inaelekea kuwa haifai kumhukumu Muislamu kuwa Muislamu hata kama kutakuwa na viashirio vingi vinavyounga mkono hukumu ya Uislamu wake madamu kuna uwezekano mmoja tu wa kugeuka kwake na kukufuru.

Basi ukafirishaji ni hukumu ya Kisharia haitolewi ila kwa dalili thabiti za kisharia, kwa hivyo marejeo yake ni katika hukumu za Sharia na fikihi ya maandiko yake, haifai katika hayo yote kuzung-

umzia bila ya elimu na ufafanuzi katoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Na kutokana na hayo, haifai kwa mlinganiaji Mwanachuoni au jamaa yeyote kuwahukumu

watu kuwa ni makafiri, jukumu hili la kuwakufurisha watu ni la Kadhi au Mufti kwa ajili ya uwezo wao wa kielimu, kwa kuzijua kukumu za Kisharia na kazi za kikadhi.

***

## Pili: Mfumo wa Utawala na Kulitumia Suala la Ukhalifa Kibiashara.

Uislamu haujaweka upande mmoja, uliogan-da, maalumu wa mfumo wa utawala ambao hai-wezekani kutoka ndani yake, bali uliweka misingi na vigezo ambavyo vikiwepo basi utawala huo huwa bora na unakubaliwa na Uislamu, na vi-napokosekena basi utawala huo huwa na mwanya na mIgongano kwa kiwango cha upungufu huo, na huwenda anuani muhimu kuliko zote na iliyo mbele ya mfumo kwa maana ya utawala bora ni upeo wa kuyafanikisha masilahi ya nchi na watu, na kwa uchache kabisa ni umbali wa kazi yake kwa ajili hiyo na juhudi zake kulekea katika masilahi hayo, kwa hivyo basi, utawala wowote unachangia kuleta masilahi ya nchi na wananchi kwa kuanga-zia maana za uadilifu, usawa na uhuru uliodhibi-tika mbali na vurugu na upendeleo wa ajira, na kutanguliza kujali uwezo, basi huo ni utawala

bora unaokubalika. Na chini ya anuani hii kuu, kunajitokeza maelezo marefu yenye lengo kwa ujumla, la kuufikia uadilifu kwa pande zake zote za kisiasa, kijamii na Kisharia kwa watu wote, na kutowabagudhi watu kwa misingi ya rangi, jinsia au kabila, na hakuna kulazimishana katika dini.

Anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu kupitia ulimi wa Mtume wake Muhammad S.A.W akiwazungumzisha makafiri nyie muna dini yenu na mimi nina dini yangu, kwa hivyo kila utawala unaofanya kazi ya kulifikia hilo na ukafanya juhudi za kutosheleza mahitaji ya msingi ya jamii, kama vile chakula, maji, makazi miundo mbinu ya afya elimu barabara na mfano wa haya, basi utazingatiwa kuwa ni uongozi bora ulio sawa na uliowafikishwa, na wenye kuridhiwa mbele ya Mola na mbele ya watu isipokuwa muono wa mwenye chuki mwenye kijicho mwenye kiburi mbishi msaliti na haini.

Na haya yanathibitishwa na Wanachuoni na watu wenye busara na wenye fikra kuwa Mwe-

nyezi Mungu Mtukufu huinusuru nchi adilifu hata kama ni ya kikafiri, na wala hainusuru nchi dhalimu hata kama ni ya Kiislamu, ama kwa wale wanaolitumia suala la Ukhalifa kama ni njia ya kujinufaisha kupitia dini na kuchezea hisia za watu kwa hoja za baadhi ya Aya ambazo wanazifasiri kimakosa bila ya kutambua fiqhi ya uhalisia na kutotambua lengo lake kwa upande mmoja, ni wakafanya huo kuwa ndiyo msingi miongoni mwa misingi ambayo kwayo hupatikana imani na ukafiri kwa upande mwingine, hakika sisi tunawajibu kwa yale ambayo ameyasisitizia Imamu mkuu Dkt Ahmad Twayib, Sheikh wa Al-Azhar Al-Sharii katika hotuba yake aliyoitoa kwenye mkutano wa "Azhar katika kupambana na ugaidi na mlengo mkali" kwamba hakana ugomvi wowote kati ya Wanachuoni wanaokubalika kuwa Ukhalifa unafaa zaidi kuwekwa katika matawi na ni karibu yake. Na madhehebu ya Ashaaira wanaona kuwa Ukhalifa ni Tawi na wala si mzizi.

Akijibu yaliyomo katika kitabu cha Sharhul Mawaagif ambacho kinazingatiwa kuwa ni moja

ya nguzo za vitabu vya madhehebu ya Ash-ariy ambapo mwandishi wake ametaja kuhusu suala la uimamu kuwa jambo hili "Si katika misingi wa Dini na Akida zote kwetu sisi bali ni tawi katika matawi miongoni mwa matawi" kisha akaelezea Imamu wetu akisema mamna namna gani jambo hili ambalo si kafika mizizi ya dini kwa Ahlu Sunna wal-jamaa, limekuwa ni tenganishi kwa vijana hawa kati ya ukafiri na imani, na fitina iliyosababisha umwagaji damu, na kubomolewa kilichojengwa, na sura ya Dini hii Tukufu kuchafuliwa!?

Mtume S.A.W. alipozungumza katika mazungumzo yake yaliyokausanya Imani, Uislamu na Ihsaan, hakuufanya ukhalifa kuwa ni nguzo miongoni mwa nguzo za Imani au za Uislamu.

Kutoka kwa Omar Ibn Khatab R.A. amesema: "Sisi tulipokuwa na Mtume siku moja alitujia mtu mwenye nguo nyeupe mno, ana nywele nyeusi haonekani kuwa na athari yeyote ya safari na hakuna yeyote kati yetu amjuaye, hadi akaa na

kupandanisha magoti yake na kisha akaweka viganja vyake juu ya mapaja yake na kasema: Ewe Muhammad nieleze kuhusu Uislamu, Mtaume S.A.W akamwambia: Uislamu ni kukiri kuwa hakuna Mola anayepaswa kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu na kwamba Muhammad ni Mtume wake, na usimamishe Swala, Utoe zaka, Ufunge Ramadhani, Uhiji Nyumba Tukufu kwa yule atakayekawa na uwezo afanye hivyo, yule Mtu akamwambia Mtume: Umesema kweli. Akasema Omar, sisi tukamshangaa, anamuualiza Mtume na kisha anamsadikisha! Akasema: Niambie kuhusu Imani, Mtume akasema Imani ni kumuamini Mwenyezi Mungu na Malaika wake vitabu vyake Mitume wake Siku ya Mwisho na kuamini kadari yake, kheri na shari yake, kisha akasema umesema kweli, Akasema: Nieleze kuhusu Ihsaan: Mtume akasema, Ihsaan ni kumuabudu Mwenyezi Mungu kama wamuona na ikiwa humuoni basi yeye anakuona. Kisha yule Mtu akasema nieleze kuhusa siku ya Mwisho, Mtume akasema, hakuwa anayeulizwa jambo hilo ni mjuzi kuliko

anayeuliza, akasema yule Mtu niambie kuhusu dalili zake, Mtume akasema ni pale kijakazi atakapomzaa bwana wake, na wakaonekana wasio na viatu walio uchi masikini wachunga mbuzi wanajenga majumba marefu, akasema Omari kisha Mtu yule akaondoka nikakaa pande kisha Mtume akaniambia, ewe Omar umamjua ni nani yule muulizaji? Nikasema Mwenyezi Mungu na Mtume wake ndio wamjuao, akasema Mtume huyo alikuwa Jibril, aliwajieni ili awafundishe dini yenu". Imepokelewa na Imamu Muslimu.

Ama jumla ya Hadithi ambazo zinazozungumzia Ukhalifa na utiifu kwa kiongozi kwa ujumla zinaweza kuchukuliwa kwa kuziangalia hali mbali mbali za katika zama zetu hizi juu ya umuhimu wa kuweka mfumo utawala adilifu na bora wenye rais na taasisi za serikali ambazo zinafanya kazi ya kuleta uadilifu kati ya watu, na kuyafikia masilahi ya nchi na ya wananchi, na unategemea ushauri na kunufaika na watu wenye uwezo wenye uzoefu na wabobezi, kwa namna ambayo watu

hawaachii mvurugano wa wasio na waangalizi wanao wadhibitisha, baada ya hapo, wala hakuna tatizo lolote juu ya majina kwa kuwa utawala huo unayatumikia malengo ambayo Uislamu unayahangaikia ili kuwapatia watu wote kwa namna ambayo inawanufaisha katika dini na dunia yao[1].

***

(1) Utafiti huo unachukuliwa kutoka kwenye kitabu cha "Nahu Tajdid Al Fikr AI-Dini" Taarifa katika Dini na Maisha, kimeandikwa na Profesa Dk. Muhamad Mukhtaar Juma. Waziri wa Mambo ya Wagfu, Uk. 115-158

## Tatu: Hakimiya: Kufuata Sharia ya Mwenyezi Mungu

Hakimiya ni: Kufuata Sharia za Mwenyezi Mungu alizoteremsha, na hii inazuia kuhukumu kwa sheria za kutungwa na binadamu katika upande wa misingi mama ya sheria na nguzo kuu, na kwa mujibu wa mabadiliko ya zama na sehemu na utumiaji wa sheria hizo za kutungwa hakuwi kinyume na Sheria za Mwenyezi Mungu kwa kuwa tu zinayatumikia masilahi makuu ya nchi na wananchi watu pamoja na jamii.

**Ubainishaji wa hayo:**

Ni kwamba makundi mbali mbali ya ukafirishaji na ugaidi yamelielewa vibaya wazo la Hakimiya ambapo makundi hayo yameingiza ndani yake yale ambayo hayakutakiwa na Sharia Tukufu ya Kiislamu.

Hakimiya ni neno lenye maana ya mfumo wa Kisharia na maana yake hasa ni kuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu ndiye Mweka Sharia Mkuu kwa viumbe wake, kwa maana kuwa Yeye ndiye anayewaamrisha na kuwakataza, anayewabalalishia na kuwaharamishia kupitia maamrisho yake ya Kisharia.

Hii ndio Hakimiya, haimaanishi kuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu Yeye ndiye anayewateuwa Makhalifa na Maamiri wahukumu kwa jinna lake, bali kinachokusudiwa neno Hakimiya ni mfamo wa Sharia tu.

Ama kwa upande wa kuegemeza madaraka ya kisiasa, jambo hili hurejeshwa kwa watu, kwani wao ndio wanaomchagua anayewaongoza na wao ndio wanaomuwajibisha na kumwadhibu, na wala Hakimiya haina maana ya wito wa dola la Theokratia yaani dola linalohukumiwa na watu wa dini.

Kwa hiyo basi, Hakimiya ya Kisharia ni ile ambayo inapaswa iwe ni ya Mwenyezi Mungu pekee,

na wala si kwa yeyote katika viumbe vyake awe ndiye, na hii ndio Hakimiya kuu, na wala haipingi mwanadamu kuwa na kiasi cha maamuzi ya Kisharia alichokiidhinisha Mwenyezi Mungu Mtakufu kwa wanadamu, na iwe ni katika mzunguko ambao kiasili hauna Aya yeyote, nacho ni kingi, nacho ni kile kilichonyamaziwa na ambacho Hadithi zimekizungumzia kwa kusema; “Na kile alichokinyamazia basi kimeruhusiwa” na mfano wa jambo hilo pia ni yale yaliyokuja katika misingi mama bila ya Hukumu ndogo na pambanuzi, na kwa hivyo watu wanaweza kujiundia sheria zao wenyewe kwa idhini ya dini yao katika nyanja nyingi tu za kijamii, kiuchumi na za kisiasa hawafungiki isipokuwa kwa malengo mama ya sheria, na yote yanachunga jinsi ya kuleta masilahi na kuondosha ufisadi pamoja na kuzilea haja za watu, iwe mtu mmoja mmoja au makundi makundi.

Na hapa tunatanabahisha kawa kanuni fafanuzi za kisasa hazipingani kiujumla na Sharia ya Kiislamu katika malengo yake mama, kwani kanuni

hizo zimejengeka kwa ajili ya kuleta manufaa na kuondosha madhara pamoja na kulinda mazoea ya kimaadili yanayopokelewa kutoka kwa babu zetu.

Na suala la kuwakafirisha viongozi kwa kutegemea kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu: ﴿**Na wasiohukumu kwa aliyo teremsha Mwenyezi Mungu, basi hao ndio makafiri**﴾ Al-Maidah: 44, ni jambo lenye kuvurugwa, ni kuwa kila anayehukumu kinyume na Sharia ya Mwenyezi Mungu Mtukufu nyumbani kwake ambako yeye ana madaraka juu ya watu wake, au katika jamii yake ambayo anaiongoza au katika taasisi ambayo yeye ndiye mkurugenzi weke, ni kafiri aliyeritadi anastahiki kuuawa kwa mujibu wa madhebebu haya ya fikra potovu.

Hakuna umuhimu wowote wa kuwepo uwezekano kuwa wao wametoa hukumu kinyume cha Sharia ya Mwenyezi Mangu kwa kuwarahisishia wao au kwa uzembe au kwa sababu ya kuelekea kwao kwenye matamanio na masilahi ya kidunia

yaliyowatenza nguvu au kwa sababu ya kulazimika kutokana na mazingira ya Ulimwengu unaowazunguka pamoja na kuwa kwao na yakini kwamba wao wako makosani kwa kuepukana kwao na kuhukumu kwa kile alichokiteremsha Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Na muonekano wa kupindukia katika jambo hili unaonekana kwa kupuuzia tofauti kati ya maasi ya kitabia ambayo hayapiti na kuwa ufuska, na maasi ya kiimani ambayo humtumbukiza muhusika kwenye shimo la ukafiri, na miongoni mwa mizizi ya Ahlu Sunna ni kuwa maasi humfanya mfu kuwa faasiki lakini hayamfanyi akawa kafiri.

Kama inavyoonekana wazi kupindukia pia katika mwelekeo wa hukumu ya kundi fulani juu ya wale wenye kujihusisha na maasi bila ya ufafanuzi au utofaufishaji, na vile vile bila ya kujali mazingira maalumu na hali za watu, na madhehebu ya Wanachuoni yamejengeka juu ya kutofautisha kati ya aina na umaalumu katika suala la ukafirishaji.

Vile vile inaonekana wazi katika kuthubutu kwenda kinyume na muongozo wa Bwana wetu Mtume wa Mwenyezi

Mungu S.A.W pamoja na kuonya kwake kutokana na kujihusisha na upindukiaji huu, na haya yapo katika Hadithi iliyopokelewa na Abu Said Al-Hudriy R.A alisema Mtume wa Mwenyezi Mungu Mtukufu S.A.W: "Watakuwa maamiri ambao nyoyo zitatulizana juu yao, na ngozi huwalainikia, kisha mtakuwa na maamiri ambao nafsi zinachukizwa nao, na nyoyo zinasimka kutokana nao, na akasema: Akasema Mtu mmoja je tupigane nao ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu? Akasema: Hapana, iwapo wataendelea kusimamisha swala«.

Hadithi hii inamaanisha kuwa kiongozi kupuuzia tu baadhi ya miongozo ya Quran na Sunna hachukuliwi kuwa ni kafiri.

Na tumekwishabainisha mwanzoni mwa kitabu hiki kuwa kuwajibika na Sharia ya Mwenyezi Mungu Mtukufu hakazuii watu kutumia sheria

walizozianda wao wenyewe mzunguko wa mizizi mama wa Muundo wa Sheria na Misingi yake Mikuu, kwa mujibu wa mabadiliko ya zama na sehemu, na kuhukumu kwa sheria hizo za kubuniwa wala hakuendi kinyume na Sharia ya Mwenyezi Mungu kwa kuwa tu kutaendelea kuyatumikia masilahi makuu ya nchi na watu wake, iwe mtu mmoja mmoja au makundi makundi.

***

## Nne: Jibadi

Waliokutana wote waliafikiana kwamba Jihadi ni: Kurudisha mashambulizi dhidi ya nchi kwa kiwango kinachofanana bila ya kupindukia au kupunguza, na hakuna nafasi ya kushambulia nchi yoyote ya wala si haki ya mtu yeyote kutangaza vita, kwani hii ni haki ya rais wa nchi pamoja na pande husika kwa mujibu wa kanuni na katiba ya nchi.

**Na ufananuzi wa hayo ni:**

Jihadi ni kufanya juhudi kwa aina zake tofauti ili kuinua neno la Mwenyezi Mungu Mtukufu na kueneza dini sahihi kati ya watu.

Na Jihadi katika Uislamu ni mti ambao shina lake ni maongeo na ulinganio kwa hekima na mawaidha bora ili kufikisha uhakika wa Uislamu sahihi kiakili, ama Jihadi ya kivita inatokana na Jihadi ya kulingania kama vile matawi yanayoto-

kana na mti, na dalili ya hayo ni kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu: ﴿**Basi usiwatii makafiri, na pambana nao kwayo kwa Jihadi kubwa**﴾ Al-Furqan: 521.

Na kiwakilishi katika kauli yake (kwayo) yaani kwa Quran, basi hiyo ni amri fafanuzi kwa Mtume S.A.W. katika Jihadi ya kuwalingania makafiri aipokuwa Makka kabla ya kuamrishwa vita.

Na Amesema: ﴿**Kisha hakika Mola wako Mlezi, kwa wale walio hama kwao baada ya kuteswa, kisha wakapiginia Dini na wakasubiri, bila ya shaka Mola wako Mlezi baada ya hayo ni Mwenye kusamehe Mwenye kurehemu**﴾ An-Nahli: 110.

Kwa hiyo Quran iliyoteremkia Makkah ina neno Jihadi na maana yake ni Jihadi ya nafsi, kwa kuwa kwake na subira ndani yake juu ya ulinganiaji, na kustahmili maudhi na kero katika njia ya ulinganiaji huo.

Baada ya kuhama kwa Mtume S.A.W. kwenda Madina, dola ya Kiislamu ilianzishwa kwa kuwepo

nyenzo zake "Katiba ardhi na Watu", na Jihadi ilihalalishwa Madina kwa ajili ya kujibu mashambulizi na kuilinda dola na nchi, na hilo ni jambo linalokubaliana na mapokeo "Mikataba" na kanuni za kimataifa.

Miongoni mwa makosa kuwa watu wengi hukubaliana kwamba sababu ya kutohalalishwa Jihadi ya kivita huko Makka ni udhaifu na sio vinginevyo, bali sababu ya kutohalalisha Jihadi katika zama za Makkah na kuhalalishwa kwake katika zama za Madina, ni kuwa Waislamu wa Makkah walikuwa hawana kitu chochote cha kukipigania, kwa hivyo, hakuna jihadi ya kivita katika Uislamu kwa ajili ya kuwalazimisha watu kuingia Uislamu. Mwenyezi Mungu Mtukufu Anasema: {Hapana kulazimisha katika Dini} na neno hakuna hapa kwa kukanusha, kama wanavyosema wanaisimu, yaani kungia kwenye dini hakuwi kwa kulazimisha, kwani dini haiwi isipokuwa moyoni tu.

Na kama ikisemwa: Basi kwanini Jihadi ya kivita haihalalishwa katika Uislamu?

Tunasema ilihalalishwa ili kujibu mashambulizi na sio kwa ajili ya kuufuta ukafiri basi mtu yeyote anaepigana na Waislamu au anashambulia nyumba na nchi zao, au nafsi zao, basi huyo ndiye tunayepigana naye, na tunajibu mashambulizi kwa ajili ya sisi kujihami.

Na kuhalalisha Jihadi hakumaanishi kwamba ndio asili ya Jihadi, na hiyo ni ulinganio kwa njia ya hekima na mawaidha bora- ikapita na ikaisha, bali ulinganio kwa Mwenyezi Mungu ulikuwa na utabakia daima kuwa ni ufunguo wa kudumu kwa namna nyingine za jihadi.

Na tofauti iliyopo kati ya Jihadi ya ulinganiaji na Jihadi ya kivita: Ni kwamba ya kwanza ni miongoni mwa hukumu za ufikishaji ujumbe. Na kwa hivyo basi, ulinganiaji hupanuka na hujibana kutokana na utamaduni wa mlinganiaji na katika msingi wa: ﴿**Mwenyezi Mungu haikalifishi nafsi yoyote Ila kwa kadiri ya uwezo wake**﴾ Al-Baqarah: 256.

Ama jihadi ya kivita: Ni miongoni mwa hukumu za siasa ya Kisharia na ni msingi katika mlango wa Jihadi kwamba Jihadi ya ulinganiaji ilikuwa na itabakia daima ni malumbano na ushawishi na siyo ulazimishaji na utenzaji nguvu, na jihadi ya kivita huwa ni kwa ajili ya kujibu mashambulizi na vita, na siyo kwa ajili ya ushambuliaji na vita.

Na haifichiki katika hayo, kauli ya Mwenyezi Mungu Mtakufu: ﴿**Na ikisha miezi mitakufu basi wauweni washirikina popote muwakutapo, na washikeni na wazungukeni, na wavizieni katika kila njia**﴾ Al-Tawbah: 05.

Na kauli ya Mtaume S.A.W amesema: "Mimi niliamrishwa kupigana na watu hadi washuhudie kuwa hakuma Mola wa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu na kwamba Muhammad ni Mtume wa Mwenyezi Mungu, na kutekeleza sala na kutoa zaka, basi wakishafanya hayo wajilinde kwa damu na mali zao nami isipokuwa kwa haki ya Uislamu, na hesabu yao ni juu ya Mwenyezi Mungu Mtukufu" wamekubaliana Mamimamu wa Hadithi.

Kwani Kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu: {Na ikisha miezi mitukufu basi wazuieni washirikina popote muwakutapo….}

ni kuhusu washirikina wanaopigana na Waislamu kwa kiashirio kilichotajwa baada yake katika kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu: {Na ikiwa mmoja wapo katika washirikina akikuomba ulinzi, basi mpe ulinzi wako apate kusikia maneno ya Mwenyezi Mungu} basi kama lengo la mapigano lingekuwa ni ukafiri pekee pasipo na kitu chochote chengine basi hiyo ingeakwenda kinyume na hukumu ya kuomba ulinzi kwa mshirikina.

Ama Hadithi imetofautisha katika lugha ya Waarabu kati ya maana ya "Naua" na maana ya "Napigana" basi uuaji si upiganaji.

Basi "Naua" maana yake: Nawafuata watu hadi katika nyumba zao ili waingie katika Uislama kwa nguvu.

Ama maana ya "Napigana" maana yake nashirikiana na wengine katika mapigano, na

maana yake ni kuwa mimi narudisha mashambulizi ya watu kwa nguvu inayofanana na ya kwao. Na Imamu Al-Baihaqiy alinukuu kutoka kwa Imamu Al-Shafiy R.A akisema: Mauaji si mapigano kwa njia yoyote ile, kwani labda inahalalisha kupigana na mtu yeyote lakini haihalalishi kumuua. Fateh Al-Baariy 76/1.

Na kama ikisemwa: Katika vita vya Mtume S.A.W watu walianza mapigano ndani yake.

Tunasema: Hakuna vita vyovyote katika zama za Mtume S.A.W. ambavyo alivianzisha Yeye kwa kushambulia.

Na kama ikisemwa: katika vita vya Khaibar Mtume aliwashitukiza kwa mashambulizi ya kuvizia.

Tunasema: Hapana, lakini alipata habari za ukweli kwamba Mayahudi wa Khaibar pamoja na kabila la Ghattafan wanapanga kuwashambulia Waislamu, basi akafunga njia yao baina ya Ghatfafan na Khaibar, kisha akaelekea Khaibar kwa

kushitukiza, katika giza nene kwa kujua kwake mapema kuwepo kwa mashambulizi ya Khaibar.

Ama vita vya Muatah: Hivi vilitokea baada ya Mtume S.A.W kumuua Al-Haarith Ibn Umair Al-Azaidiy na kupenga kwao kuwashambulia Waislamu.

Na katika vita vya Tebouk: Ni kuwa baadhi ya wafanyabiashara Wagiriki waliwaambia baadhi ya Waislamu kwamba Wagiriki wanapanga kuwashambulia Waislamu.

Ama ufunguzi wa Shamu na Misri: Ni kwamba ulitokana na mwelekeo wa Wagiriki madhalimu walioimwaga damu ya Wamisri na watu wa Shamu, mpaka wakazi wa nchi hizo wakaamua kuwakaribisha Waislamu, basi Waislamu hao wakaziingia nchi hizo bila ya mapigano.

Swali: Je, ufunguzi wa Uislamu ulimlazimisha matu yeyote miongoni mwa Wamisri au watu wa Shamu kuingia katika Uislamu?

Jawabu: Hapana, kwani kama jambo hili lingekuwa hivyo asingebakia mtu yeyote asiye kuwa Muislamu katika nchi walizoziingia

Waislamu, bali Waislamu walipoingia nchi hizo hawakumlazimisha mtu yeyeote miongoni mwa watu wake kuingia kaitka Uislamu, kwa kuwa misingi katika Sharia ya Kiislamu ni kuishi pamoja na wengine kwa maelewano ushirikiano na utulivu daima. Mwenyezi Mungu Mtukufu Anasema: ﴿**Mwenyezi Mungu hakukatazeni kuwafanyia wema na uadilifu wale ambao hawakukupigeni vita, wala hawakukutoeni makwenu. Hakika Mwenyezi Mungu huwapenda wafanyao uadilifu * Hakika Mwenyezi Mungu anakukatazeni kufanya urafiki na wale walio kupigeni vita, wa wakakutoeni makwenu, na wakasaidia kafika kufukuzwa kwenu. Na wanaowafanya hao kuwa marafiki basi hao ndio madhaalimu**﴾ Al-M umtahinah: 8, 9.

***

## Tano: Utaifa.

Utaifa: Neno hili lina maana kuwa wananchi wote ni sawa kwa haki na wajibu ndani ya mipaka ya nchi yao.

**Na ufafanuzi wa hayo:**

Uraia ni: Ushirikiano wa kiutendaji kati ya mwananchi na nchi ambayo yeye anaishi ndani yake na ana uhusiano nayo. Na uraia unataka uhusiano na uzalendo wa mwananchi huyu vikamilike kwa ajili ya nchi ambapo anafakiwa aheshimu utambulisho wake, na ajiamini na ahusiane nayo na awe tayari kuilimda wakati wowote.

Na huo uhusiano wake na nchi unaafikiana na kaulii ya kwamba, upendo wa mwanadamu kwa watu wake na nchi yake ni upendo wa kimaumbile, unazaliwa na mwanadamu mwenye maumbile yaliyosalimika ambapo mataifa mbali mbali

yenye tofauti za kikabila, kilugha na mila na desturi, yanashirikiana katika jambo hili. Na maana hii imetajwa katika baadhi ya misemo ambayo inasisitizia upendo wa nchi na kushikamana nazo na kuzilinda kama vile msemo wa wahenga usemao: "Kupenda nchi ni sehema ya imani" na msemo wao mwingine: "Ukitaka kujua uaminifu wa mtu fulani basi angalia shauku yake kwa nchi yake".

Na hayo yanatuashiria kutopingana mafungamano ya mtu na nchi yake pamoja na wananchi wenzake, na mfungamano wa Akida na Dini, kwani dini na mafunzo yanayomwagiza mwanadamu kuhifadhi mafungamano hayo ambayo yana unda utambulisho wa kitaifa.

Na mfungamano huu kati ya utambulisho wenye pande mbili unaungwa mkono katika Uislamu: Ni kwamba Sharia imewajibisha vita vya ulinzi wa nchi na watu, na inamzingatia anayeuliwa kwa ajili hiyo kuwa ni shujaa aliyekufa shahidi.

Kwa hiyo, uraia unawakusanya watu wote ambao wanaishi katika nchi moja bila ya kuwatofauti-

sha, na unawajibisha usawa kati ya yao katika haki na wajibu ambapo yote hutokana na uhusiano huu wa kitaifa,

Na hayo yanadhihirika wazi katika Hati Tukufu ya Madina ambayo Mtume S.A.W aliziunda pamoja na pande zote mbalimbali za kijamii ndani ya Madina, mwanzoni mwa zama mpya za kuunda Dola na kupangilia mambo yake. Na Madina ilikuwa ni makazi ya Makabila mawili ya Al-Ausi na Al-Khazraji, Mayahudi, Wahamiaji na watu wengine. Na Utambulisho wa kidini ulikuwa tofauti kati ya watu hao wote, lakini Utambulisho wa nchi ulikuwa unawakusanya wote kwa pamoja.

Na Hati hiyo iliwalinganisha watu wote kuwa ni sawa kwenye ubinadamu wao na katika haki na aina mbali mbali za uwajibikaji wa kitaifa, wakiwemo Mayahudi na wengineo ambao hawakuamini ujumbe wa Kiislamu. Na Hati hiyo ya Madina ilijumuisha mkataba wa kijamii ulianzisha misingi ya kiundugu kati ya wahamiaji na wenyeji na ukay-

alinda maisha ya pamoja kati ya Waislamu na watu wengine miongoni mwa wananchi wanaoshirikana nao utaifa katika wale ambao hawakuamini ujumbe wa Kiislamu.

Na Hati hiyo iliwapa haki ya usawa pamoja na Waislamu katika masilahi ya umma, na ikawadhamini kwa haki zao zote za ibada na aina mbali mbali za uhuru wao binafsi, mila na desturi zao, juu ya msingi wa kuishi pamoja na mshirika wao katika nchi, na kwa kunufaika na kauli ya Menyezi Mungu Mfukufu isemayo: ﴿**Mwenyezi Mungu hakukatazeni kuwafanyia wema na uadilifu wale ambao hawakukupigeni vita, wala hawakukutoeni makwenu. Hakika Mwenyezi Mungu huwapenda wafanyao uadilifu**﴾ Al-Mumtahinah: 08.

Hati hiyo ilikuwa na maelezo yanayosema kuwa: Mayahudi wa Madina pamoja na Waislamu ni umma mmoja, kwani Wayahudi wana dini yao na Waislamu wana dini yao, kwa msingi wa kuishi pamoja kibinadamu na kwa amani.

Neno “Watu wa dhima” kwa sasa lina maana ya neno “Uraia na mwananchi”, kwa hivyo basi, uraia unamaanisha kuwa Waislamu na wasio Waislamu wanaishi katika ardhi moja, na uraia na sehemu walipo vinawakusanya. Kwa hivyo basi, wasio Waislamu wana haki kamili za utaifa, na jukumu la utawala linabebwa na Waislamu na wasio Waislamu pia, Kwa hivyo basi, nchi ni miliki ya wote, na wote ni sawa, kwa wale wanaotetea ndani yake Itikadi yao, na wale ambao wanatetea ndani yake ardhi na heshima ya nchi yao.

***

## Sifa: Ugaidi

Ugaidi ni uhalifu wa kupangwa unaohusisha kikundi cha watu waliokiuka mfumo wa Dola na jamii yao, na husababisha umwagaji damu za watu wasio kuwa na hatia au kuharibu taasisi au kushambulia mali za umma au za watu binafsi.

**Ufafanuzi wake:**

Uwepo wa ugaidi unazingatiwa kuwa ni muonekano ulio hatari mno ambao unaweza kuikumba jamii yoyote miongoni mwa jamii mbali mbali ambapo athari zake huzigusa nyanja zote kuu za kimaisha: Siasa Uchumi Jamii na nyenginezo.

Na Uislamu umekataza Ugaidi, kwani Uislamu ni dini ya amani kwa watu wote, kwa hivyo hauwezi kamwe kuwa pamoja na matumizi ya nguvu na uadui, kwani viwili hivi ni kinyume cha Uislamu, na Waislamu wanaamrishwa kuanza na

maamkizi kwa kila mtu wanayekutana naye na maamkizi ya Kiislamzu ni tamko la amani huruma na utulivu wa kueneza usalama kwa watu wote.

Kwa hivyo vinyume viwili haviwezi kukutana: Amani na matumizi ya nguvu, bali ni kwamba Waislamu wameamrishwa kutafuta amani na kuielekea iwapo adui ataamua kufanya hivyo na akawa na utashi wa kweli ndani yake, na hii ni katika hali ya vita iliyotangazwa, sasa itakuwaje iwapo hapatakuwepo vita ya aina yeyote! Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema: ﴿**Na wakielekea amani nawe pia elekea, na mtegemee Mwenyezi Mungu. Hakika Yeye ndiye Mwenye kusikia Mwenye kujua. Na wakitaka kukuhadaa basi Mwenyezi Mungu atakutosheleza. Kwani Yeye ndiye aliye kuunga mkono kwa nusura yake na kwa Waumini**﴾ Al- Anfaal: 61-62.

Na kwa kuwa ulazimishaji ni moja kati ya aina za ugaidi, hakika Uislamu unaupiga vita kwa kila sura zake na aina zake, kwani kulazimisha hupelekea matokeo ya kinyume na inavyotarajiwa, na kusambaza unafiki ambao ni msingi wa uhaini, hi-

yana na kutafutana, hata katika masuala ya kuingia katika Uisamu, kwani Mwenyezi Mungu Mtukufu hakuweka Sharia ya kuwalazimisha watu kuingia kwenye Uislamu, Akasema: ﴿**Hapana kulazimisha katika Dini Kwani Uwongofu umekwisha pambanuka na upotofu, basi anaye mkataa shetani na akamuamini Mwenyezi Mungu bila ya shaka amekamata kishikio madhubuti kisicho vunjika. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia, Mwenye kujua**﴾ Al- Baqaraha: 256.

Na Uislamu umeharamisha mauaji na umwagaji damu ya mtu mwenye kinga ya Uislamu, na ukalifanya jambo hili la mauaji kuwa ni moja kati ya madhambi makubwa: Mwenyezi Mungu Mtukufu Anasema: {Wala msiuwe nafsi ambayo Mwenyezi Mungu amekataza isipokuwa kwa haki, Na aliye uliwa kwa kudhulumiwa basi tumempa madaraka mrithi wake. Lakini asipite mpaka katika kuuwa, Kwani yeye anasaidiwa} Al- Israa: 33.

Na amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu: ﴿**Kwa sababu ya hayo tuliwaandikia wana wa lsraeli ya kwamba aliye muuwa mtu bila ya**

**yeye kuuwa, au kufanya uchafuzi katika nchi, basi ni kama ameuwa watu wote, na mwenye kumuokoa mtu na mauti ni kama amewaokoa watu wote, na hakika waliwajia Mitume wetu na hoja zilizo wazi, kisha wengi katika wao baada ya haya wakawa waharibifu katika nchi**﴾ Al-Maidah: 52. Na Amesema: ﴿**Na mwenye kumua Muumini kwa kukusudia, basi malipo yake ni Jahannamu hamo atadumu, na Mwenyezi Mungu amemkasirikia, na amemlaani, na amemuandalia adhabu kubwa**﴾ An- Nisaa: 93.

Na kutoka kwa Abu Huraira R.A amesema: Mtume S.A.W amesema: "Jiepusheni na mambo saba yenye kuangamiza, akaulizwa ni yepi hayo ewe Mtume wa Mwenyezi Mangu? Akasema: Ni kumshirikisha Mwenyezi Mungu, uchawi, kuuwa nafsi ambayo Mwenyezi Mungu ameharamisha isipokuwa kwa haki, kula mali ya yatima, kula riba, kukimbia siku ya vita, na kuwatuhumu uzinzi wanawake wenye kuzilinda tupu zao Waumini". Imepokelewa na Imamu Bukhariy.

Na kutoka kwa Abdullahi Ibn Omar R.A amesema: Mtume S.A.W. amesema: “Muumini ataendelea kuwa na nafasi kubwa ya dini yake iwapo hatamwaga damu iliyeharamishwa kumwagwa«. Imepokelewa na Imamu Bukhary.

Na amesema Ibn Omar R.A “Hakika miongoni mwa maovu ya kujiingiza (mtu) ambayo mtu aliyeitumbukiza nafsi yake hawezi kuitoa, ni umwagaji wa damu ambayo imeharamishwa kumwagwa bila uhalali wa kufanya hivyo”.

Na Uislamu umeharamisha kuwatishia walio salama, hukumu za Kisharia zimekuja kwa ajili ya kuzuia vitendo ambavyo vinawatisha na kuwatia woga watu walio na usalama. Na kwa katazo hilo kuna zuia pia kuashiria kwa silaha. Na katika Hadithi kutoka kwa Abu Huraira R.A kwamba Mtaume S.A.W. Amesema: “Yeyote atakayemuashiria ndugu yake kwa silaha hakika Malaika watamlaani hadi atakapoacha kufanya hivyo hata kama (Anayeashiriwa silaha) ni ndugu yake wa kuzaliwa, baba mmoja mama mmoja”.

Na Sharia ya Uislamu imepevuka katika namna ya kumtendea asiyekuwa Muislamu kwa kiwango cha juu mno ambacho hakuna sheria zozote miongoni mwa sheria za kibinadamu na mfumo wowote miongoni mwa mifumo iliyowahi kufikia kiwango hicho, kwani Sharia hii ya Kiislamu imewalindia haki zao za kiuchumi, kimaadili na kijamii, kama ambavyo pia imezilinda mali zao, roho zao na hata heshima zao, na wala haikuwalazimisha kuacha dini yao na chochote kilicho chini zaidi ya hivyo.

Na Quran Tukufu imeelekeza kuwatendea wema na kushirikiana nao kwa wema, bali kuwa wema kwao na kuwafanyia uadilifu. Anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu: ﴿**Mwenyezi Munga hakukatazeni kuwafanyia wema na uadilifu wale ambao hawakukupigeni vita, wala hawakukutoeni makwenu. Hakika Mwenyezi Mungu huwapenda wafanyao uadilifu...**﴾ Al-Mumtatahinah: 08.

Na Mtume S.A.W amesisitizia kiapo cha adhabu na akaweka adhabu kali mno kwa atakaye halalisha damu ya wasio kuwa Waislamu na iliyoharamishwa kumwagwa au kuwaudhi, na akasema S.A.W: "Atakayemuua mwenye ahadi na Waislamu hatanusa harufu ya Pepo, na hakika harufu yake hupatikana umbali wa mwendo wa miaka arubaini". Imepokelewa na Imamu Bukhary.

Sharia ya Kiislamu imezuia kupindukia katika dini, na ikawaonya Waislamu kufanya hivyo ili wasije wakapotea na kupotoka, kwani kupindukia katika dini ni njia inayopelekea fikra na imani kali.

Na uelewa mbaya wa dini unaweza kumsukumia mtu katika kujaribu kulazimisha kwa nguva kile anachokiamini yeye, na jambo hili ndilo linalothibitishwa na uhalisia wa hali inayoonekana kwa sasa.

Na Mwenyezi Mungu ameujaalia umma wa Kiislamu kuwa ni wa kati na kati kwa sababau dini yao iko hivyo: Amesema Mwenyezi Mungu Mtu-

kufu: ﴿**Na vivyo hivyo tumekufanyeni muwe Umma wa kati na kati, ili muwe mashahidi juu ya watu, na Mtume awe ni shahidi juu yenu...**﴾ Al- Baqarah: 143.

Kwa hivyo upindukiaji ni kinyume cha msimamo wa kati na kati, na ikiwa ukati na kati una maana na uwiano katika mambo yote, kwa hivyo upindukiaji una maana ya ugumu na ukandamizaji wa nafsi kwa kuifuata njia moja iliyo mbali na ukati na kati, na ukati na kati wa Uislamu ni uwiano kati ya hukumu zote, kwa hivyo hakuna upindukiaji na ukali, uachiaji na uzembe, na kwa hivyo hakuna kuzidisha wala kupunguza katika Uislamu.

Na ukati na kati wa Uislamu ni ngao ya jamii dhidi ya sumu ambazo zinaweza kuwepo kwa sababu ya ukandamizaji wa wenye misimamo mikali ambao wanategemea mtazamo finyu wa ulimwengu na maisha, na huanzia katika mtazamo wao huo katika kukosoa kila rai inayokwenda kinyume na yao, kwa jina la dini, na huitia makosani kila fi-

kra inayokwenda kinyume na fikra yao kwa jina la dini, jambo ambalo huwafanya wao kuishia katika kuwakufurisha watu, au hata kuwavunjia heshima Wanachuoni na kuwapa sifa mbaya wasizostahiki hata kidogo. Kwa hivyo upindukiaji katika dini ni mlango mkali unaosababisha matumizi ya nguvu na kuhangaikia katika kumlazimisha yule anayekwenda kinyume nao afuate rai kinyume na rai yake kwa nguvu.

Na Uislamu umeweka Sharia kwa kila ambaye nafsi yake itamtuma atoke na kuendeleza juhudi zake za kueneza uovu duniani, au kwa kufedhehesha na kitisha, kuuwa na kuangamiza.

Kwa kiivyo ni lazima pawepo mipaka na adhabu kali, na njia ambazo zitasaidia kung'oa mizizi ya Ugaidi katika Jamii zetu, na kumzuia kwa adhabu kali kila mtu anayefanya kitendo chochote ambacho kinavuruga usalama wa watu na amani yao. Na miongoni mwa adhabu za kutangulizwa: Ni adhabu ya Hiraba: ambayo ni vita dhidi ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Na ufafanuzi

wake umekuja katika tamko la Mwenyezi Mungu pale Aliposema: ﴿**Basi malipo ya wale wanao mpiga vita Mwenyezi Mungu na Mtume wake na wakawania kufanya uchafuzi katika nchi, ni kuuwawa, kusalibiwa, kukatwa mikono yao na miguu yao kwa mabadilisho, au kuondolewa nchini, hii ndiyo fedheha yao kafika dunia na akhera watapata adhabu kubwa**﴾ Al-Maidah: 33.

Na Hiraba imeelezwa kwa maelezo ya aina mbili ambayo ni: Kumpiga vita Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na kufanya uharibifu na kuueneza katika ardhi. Na aina hizi mbili za maelezo zinapelekea kuainisha katika kihalifu kwa kutoka nje ya hukumu za Sharia ya Kiislamu, kwani kupigana na Mwenyezi Mungu na Mtume wake S.A.W ambako kunapatikana katika Aya hii iliyotajwa si kwa uwazi wa Aya kwani kinachokusudiwa kwayo ni kuchukua hatua za kufanya vitendo vya kihalifu vinavyokwenda kinyume na hukumu za Mwenyezi Mungu na kutoka katika Mfumo wa Mtume S.A.W. kwa uadui muovu dhidi ya watu na dhidi ya nafsi zao na mali zao.

Na Hiraba inaafikiana na kile kilichopewa jina la ugaidi katika zama za kisasa kwa kuwa katika ugaidi kuna kubeba silaha kuwatisha watu na kutoka katika Sharia. Na mjongeleano huu wa sifa ya wazi unapelekea kuwepo mfanano wa namna ya kutoa adhabu baada ya kuwepo masharti yote yanayohitajika ili kutolewa hukumu kwa muhusika wa uhalifu huu, na kutekelezwa adhabu kama hizi ndio njia ambayo inaweza kuondosha chanzo cha ugonjwa huu wa kukata njia zake. Kinachotakiwa ni kuwepo kwa hukumu ya Mahakama, na kutekelewa na vyombo husika, na wala si watu miongoni mwa watu au watu wote kwa ujumla wao.

***

## Saba: Jizyah: - Kodi Maalumu

Hili ni jina la jukumu la kifedha ambalo halipo kwa wakati wetu kwa na imetoweka kutokana na kutoweka kwa jambo lililopelekea kuwepo Kisharia kwa ajili yake katika zama zetu, kwa kuwa wananchi wote wamekuwa sawa kwa haki na wajibu, na sehemu yake ikachukuliwa na njia nyengine za kisheria na taratibu za kifedha na kupelekea kutoweka kwa sababu ya kuwepo kwake.

Na yaliyokuja katika Ouran kuhusu kodi hii yanawahusu maadui na wapiga vita Waislamu na wanaoukana utaifa wao katika nchi ya Kiislamu, na si kwa wananchi walio salama na ambao washiriki katika ujenzi wa taifa na ulinzi wake,

**Ufafanuzi wake:**

Al-Jizyah (kodi) ni malipo yaliyowekwa na Dola la Kiislamu kwa wale walioingia ndani ya Dola hilo bila ya kuingia katika Uislamu, na wala

kodi hii haikuwa ni ugunduzi wa Kiislamu, bali ilikuwa ni kodi inayojulikana katika sheria zilizotangulia Uislamu, na ambayo ilikuwa ikitolewa kwa sababau za kutokuingia jeshini na kuilinda nchi na raia wake.

Kwa hivyo ikawa badala ya mafunzo ya kijeshi, na wala haijawahi kuwa badala ya imani ya Uislamu... na ushahidi ni kuwa kodi hii haijawahi kewekwa isipokuwa kwa wenye uwezo wa kuingia jeshini, na wana uwezo wa kuilipa kwa ajili ya kutopelekwa jeshini. Na kama ingelikuwa badala ya imani ya Uislamu basi ingelikuwa lazima kwa wote wasio Waislamu bila ya kubagua, lakini haikuwa hivyo, kwani kodi hii haijawahi kuwekwa kwa wazee, watoto, wanawake na vikongwe au wagonjwa miongoni mwa watu wa Kitabu Wayahudi na Wakristo, pia kodi hii haikuwekwa kwa watawa na viongozi wa kidini, na Wanachuoni wote wa Kiislamu - ukiwatoa Wanachuoni wa madhehebu ya Imamu Maliki - wamesema: Kodi hii hutolewa kwa ajili ya ukombozi na Jihadi.

Kodi hii iliwekwa kwa wenye uwezo - kimwili na kifedha - miongoni mwa Wakristo wa Najraan kwa mkabala wa kuwaachia wasiingine jeshini. Mtume S.W.A amesema kuhusu jambo hili: “Hakuna mtu yeyote miongozi mwa watu wa dhimma atakayelazimishwa kutoka kwa Waislamu na kuelekea kwa adui wa nchi ili kupambana naye vitani, na kupambana na wenzi wao, na Waishamu wawe wapiganaji kwa niaba yao, na walinzi wao kuliko watu wengine«.

Na katika nchi ambayo wasio Waislamu walijitolea kijeshi pamoja na Waislamu, hakuna kodi yeyote iliyowekwa kwao wailipe, bali walikuwa sawa sawa na Waislamu vitani na katika mgao wa ngawira, kama ilivyotokea katika tukio la Jarjaan, ambako mkataba wa kiongozi ambaye ni Suweid Ibn Muqrin aliouweka na watu wake unasema: “Na yeyote kati yenu atakayetusaidia basi ana malipo yake kutokana na msaada wake huo”. Na tukio kama hili lilitokea pia kwa Wakristo wa Humsu, walipopigana vita wakiwa pamoja ma wa-

najeshi wa jeshi la Abu Ubaida Ibn Jaraah kafika eneo la Yarmuuk dhidi ya Warumi wa Byzantine,

Omar Ibn Khattab naye aliwaondoshea kodi hii Wakristo wa ukoo wa Taghlab baada ya kuona namna wanavyoichukia na kulazimika kuilipa bila kupenda, na wala hakuwa na uhakika wa kutojitenga kwao na kujiunga na Warumi, ili wawasaidie wao dhidi ya Waislamu na akatambua kuwa hakuna madhara yeyote kwa Waislamu kuifuta kodi hiyo, na akawaondoshea. Na akaichukua kutoka kwao kwa jina la sadaka pale alipowaongezea kiwango chake. Imepokelewa na Ibn Salaam katika mlango wa Mali, na Abu Yusufu katika mlango wa malipo ya kadi.

Ama kwa kile ambacho Quran imekiita kuwa ni madhalili, ni kwamba imekiweka juu ya Hiraba na sio kwa kukufuru tu au kwa kujinasibisha na watu wa Kitabu, na pindipo vita dhidi ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake vinapokwisha basi hakuna tena Madhalili hao.

Na Wanachuoni wameitilia mkazo Sharia kali kwa yule anayewafanyia ubaya watu wa Kitabu kwa aina yeyote miongoni aina ya ushirikiano, bali wakasisitiza umuhimu wa kushirikiana naye vizuri na kuwatendea wema.

***

## Nane: Nyumba ya Uadui

Nchi ya Adui: ni ile nchi ambayo imeishambulia nchi ya Kiislamu, na rais wa nchi iliyoshambuliwa akatangaza kuchukua hatua za kuilinda nchi yake, kwa hivyo nchi adui wakati huo ndio inaitwa Daarul-Harbi (Nyumba ya Uadui) na kama hapakutokea kati ya nchi yeyote na Waislamu mapigano au uadui basi nchi hiyo huitwa nchi ya Usalama.

Inaeleweka kwamba kila nchi ambayo inakuwa na uwakilishi wa kidiplomasia kati yake na nchi ya Kiislamu basi inaingia katika jina la nchi ya amani, pia Mabalozi, watalii, na wafanya biashara ambao wanaingia katika nchi ya Waislamu ni kwamba wao wote ni watu wa ahadi na usalama na haifai kuwagusa au kuwatawanya, bali ni lazima kuwakirimu na kuwatendea wema kwa kuwa tu wanafuata sheria zilizoandaliwa kwa ajili ya kuingia kwao na kuishi katika nchi yetu.

Wanapokiuka sheria hizo basi kuwachukulia hatua ni kazi ya serikali na si ya watu tu, kwa mujibu wa makubaliano ya kimataifa na mahusiano ya kidiplomasia.

Isipokuwa wenye siasa kali wanang'ang'ania kuwa nchi ya kafiri lazima iwe daima ndio nchi ya adui. Hakuna nafasi ya mkataba au usalama wanaowajibika nao Waislamu kwa kuwa tu watu wa nchi hiyo ni makafiri.

Na atakayeweza miongoni mwa Waislamu kupora mali zao na kuzitwaa kwa nguvu basi na afanye hivyo. Na kwa mtazamo huu, dunia nzima itakuwa ni nchi ya vita (Nchi ya adui) kwa mtazamo wao hawa wenye siasa kali na kuzidisha, Hata nchi za Kiislamu kwa mtazamo wao hawa, ni nchi ya vita, kwa kuwa watu wake hawatekelezi Sharia ya Mwenyezi Mungu ndani ya nchi hiyo, na wasio kuwa Waislamu ni wapiga vita Uislamu kwa sababu ni makafiri. Na hivi ndivyo dunia nzima inavyogeuka na kuwa ni nchi ya adui na kuuwa na kupigana kwa mtazamo wa hawa magaidi.

Na mtazamo huu umeigeuza dunia na kuwa uwanja wa mapambano, badala ya moyo wa maongezi ya kistaarabu na kumkubali mwengine pamoja na kuishi naye kwa amani ambayo Dini yetu Tukufu imeweka na kuimarisha misingi yake, ambapo Hati ya Madina inazingatiwa kuwa ni Hati muhimu mno ya kibinadamu katika Fighi ya kuishi pamoja kibinadamu pamoja na kutofautiana dini, imani na asili za kimaumbile.

***

## omoyilaY


| | |
|---|---|
| Utangulizi. | 5 |
| Nyasia za Mkutano wa Kimataifa wa ishirini na nne wa Baraza Kuu la Mambo ya Kislamu (Ubainishaji na uchambuzi) | 7 |
| Dibaji | 21 |
| Uainishaji wa Mieleweko na marejeo yake ya Kisharia Kwanza: Ukafirishaji: | 29 |
| Pili: Mfumo wa Utawala na Matumizi ya Kibiashara ya Suala la Ukhalifa | 39 |
| Tatu: Ufuasi wa Sharia ya Mwenyezi Mungu:) | 47 |
| Nne: Jihadi | 55 |
| Tano: Uraia | 65 |
| Sita: Ugaidi | 71 |
| Saba: Kodi | 83 |
| Nane: Nchi ya Adui (Inayopigana na ya Waislamu) | 89 |

Shirika Kuu la Vitabu la Misri.

Msimamizi wa miradi ya kitamadani.

**Marwan Hamad**

**Mkaguzi**

**Faryal Fuad**

Mtangenezaji wa jarada la kitabu

**Muhammad Baghadady**

**Upande wa Ufundi**

**Mirfat Antar An-Nuhas**

Namba ya kuhifadhia kwenye kitengo cha vitabu 2021

SIBN